## 24- Faharasa

| Neno | Maana Yake |
|---|---|
| *'Arafah* | Sehemu muhimu kabisa ya kusimama katika Hajj ambayo ndio kilele cha Hajj, na bila yake Hajj haikamiliki. Iko baada ya *Muzdalifah* kutoka Makkah, na jabali lake huitwa Jabal *'Arafah*. |
| *Al-Baqiy'* | Sehemu Madiynah ambako kuna makaburi ya Maswahaba. |
| Al-Haaj | Mwanaume mwenye kutekeleza fardhi ya Hajj huko Makkah. Lakini haifai kuitwa baada ya kurudi nyumbani. |
| Al-Haajah | Mwanamke mwenye kutekeleza fardhi ya Hajj huko Makkah Lakini haifai kuitwa baada ya kurudi nyumbani |
| *Al-Hajar Al-As-wad* | Jiwe jeusi lilioko pembeni mwa *Al-Ka'bah*. |
| *Al-Haram* | Sehemu tukufu kama *Masjid Al-Haraam*, *Masjid An-Nabawiy*, *Mash'ar Al-Haraam* (*Muzdalifah*). |
| *Al-Idhwtiba'a* | Kuweka sehemu ya katikati ya shuka (Ridaa) chini ya kwapa ya mkono wa kulia na ncha zake juu ya bega la mkono wa kushoto katika *Twawaaf*. |
| *Al-Ifraad* | Aina ya Hajj inayotekelezwa bila ya 'Umrah. Mahujaji hahitajiki kuchinja. |
| *Al-Jamrat Al-'Aqabah* | Nguzo kubwa ya Jamrah (kurusha vijiwe) iliyoko karibu na Makkah. |
| *Al-Jamrat Al-Wustwaa* | Nguzo ya katikakati ya Jamrah (kurusha vijiwe) iliyoko *Minaa* |
| *Al-Jamrat Asw-Swughraa* | Nguzo ndogo ya Jamrah (kurusha vijiwe) iliyoko *Minaa* |
| *Al-Ka'bah* | Nyumba tukufu iliyoko katika Msikiti mtukufu wa Makkah. |

| | |
|---|---|
| *Al-Mar-wah* | Jina la jabali ambako Muislamu anamalizia *As-Sa'-y* yake. |
| *Al-Mas-'aa* | Eneo la kufanya *As-Sa'-y* katika *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* |
| *Al-Qiraan* | Hajj anayotekeleza mtu kwa kuunganisha 'Umrah na Hajj bila ya kujitoa katika Ihraam. Mahujaji huwa amefika Makkah akiwa na mnyama wa kuchinja. |
| *Ar-Rakdhw* | Kukimbia katika *As-Sa'-y* baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* kwenye alama za kijani. |
| *Ar-Raml* | Kwenda mwendo wa mbio mbio kwa hatua ndogo ndogo katika mizunguko mitatu ya mwanzo kwenye *Twawaaf*. |
| *Ar-Ram-y* | Kurusha vijiwe. |
| *As-Sa'-y* | Kutembea baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*. |
| *As-Sa'-y* | Kutembea baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*. |
| *Asw-Swafaa* | Jina la jabali ambako Muislamu anaanza *As-Sa'-y*. |
| *Asw-Swiraatw* | Njia watakayopita watu Siku ya Qiyaamah kuingia katika Jannah au kuangukia Motoni. |
| *Atw-Twawaaf* | Kuzunguka *Al-Ka'bah* mara saba. |
| *Ayyaam Al-Biydhw* | Masiku meupe ya mwezi unapokuwa umejaa katikati ya mwezi yaani tarehe 13, 14 na 15 za kalenda ya Kiislamu. |
| *Bid'ah* | Uzushi – kitendo au 'amali inayotekelezwa bila ya kuthibiti dalili yake kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم), Maswahaba na *Salafus-Swaalih*. |
| *Burqah* | Aina ya niqaab ya kufunika uso kwa wanawake. |
| *Dhul-Hijjah* | Mwezi wa kumi na mbili katika kalenda ya Kiislamu. |
| *Dhul-Qa'dah* | Mwezi wa kumi na moja katika kalenda ya Kiislamu |

| | |
|---|---|
| *Du'aa* | Kumuelekea Allaah (سبحانه وتعالى) katika kuomba haja. |
| *Ghashwah* | Mtandio au shungi jepesi la kufunika uso bila ya kubanika uso. |
| *Ghayr Muakkadah* | Isiyosisitizwa. Mfano Swalaah za kabla ya Swalaah ya Alasiri au rakaa mbili kabla ya Magharibi na 'Ishaa. |
| *Ghuslu* | Josho. Kuoga kwa ajili ya kujitwaharisha janaba, hedhi, nifaas au kuoga kwa ajili ya Ijumaa, kumwosha maiti. |
| *Hajj Mabruwr* | Hajj iliyofanikiwa ambayo jazaa yake ni Jannah. |
| Hamzah | 'Ami yake Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliyekufa Shahiyd katika vita vya Uhud. |
| *Haniyfaa* | Kuelemea upande mmoja tu wa haki na kujiengua na ubatilifu. Sifa ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) Amempa Nabiy Ibraahiym (عليه السلام). |
| Hedhi | Damu anayopata mwanamke kila mwezi |
| *Hijr* | Sehemu iliyoko pembezoni mwa *Al-Ka'bah*. Wengi wanaiita kimakosa kuwa ni '*Hijr* Ismaaiyl' na hali inapaswa itajwe kuwa ni *Hijr* pekee kwani ni sehemu ya *Al-Ka'bah*. |
| *Ihraam* | Kuingia katika niyyah ya 'ibaadah ya Hajj au 'Umrah. Shuka mbili wanazovaa wanaume katika hali hiyo pia huitwa hivyo. |
| *Ikhlaasw* | Kusafisha niyyah na 'amali kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee. |
| Istilaam | Kuligusa kwa mkono *Al-Hajar Al-As-wad* katika kutufu *Al-Ka'bah* na mtu akishindwa kulifikia ni kuashiria kwa mkono na hivyo ni kama kuliamkia. |
| *Istiqaamah* | Kuthibitika katika 'Ibaadah na 'amali njema. |
| *'Iyd Al-Adhw-haa* | Sikukuu ya kuchinja yaani 'Iyd katika mwezi wa Dhul-Hijjah. |
| *Jaahiliyyah* | Wakati wa ujinga yaani kabla ya Uislamu. |

| | |
|---|---|
| *Jabal Al-Hiraa* | Jabali alilokuwa akikaa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kutafakari na akateremshiwa Wahyi wa mwanzo kabisa. |
| *Jabal Ath-Thawr* | Jabali alojificha Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) na Abu Bakr (رضي الله عنه) wakati walipokuwa wakifanya hijrah kuelekea Madiynah, wakalifikia Makafiri wa ki-Quraysh mlangoni mwake ila Allaah (سبحانه وتعالى) Aliwalinda kwa Qudra Yake. |
| *Jamaraat* | Ujumla wa Jamrah – Minara wanayorushia vijiwe Mahujaji. |
| *Kaffaarah* | Fidia ya kuchinja au kufunga Swawm au kutoa sadaka, au kulisha masikini au kuacha huru mtumwa n.k. |
| *Khushuu'* | Unyenyekevu unaokusudiwa khasa katika Swalaah kwa kusilimisha akili, moyo na viungo kumnyenyekea Allaah (سبحانه وتعالى). |
| *Lawh Al-Mahfudhw* | Ubao Uliohifadhiwa ambao umeandikwa na Allaah (سبحانه وتعالى) *Qadhwaa* na *Qadar*. |
| *Manaasik* | Matendo ya Hajj au ya 'Umrah. |
| *Maqaam Ibraahiym* | Jiwe alilokanyaga Nabiy Ibraahiym na kusimama kuomba Du'aa baada ya kujenga *Al-Ka'bah*. |
| *Mas-'aa* | Eneo lilonyooka baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*. |
| *Mas-h Al-Khuffayn* | Fiqhi ya wudhuu kuhusu kupangusa juu ya soksi za ngozi zilizovuka makongo mawili ya miguu kwenda juu, au hata soksi za kawaida au viatu kwa ajili ya kutekeleza wudhuu. |
| *Mash'ar Al-Haraam* | Bonde tukufu lililoko *Muzdalifah*. |
| *Masjid Al-Haraam* | Msikiti Mtukufu wa Makkah. |
| *Masjid An-Nabawiy* | Msikiti wa Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) – Madiynah. |
| *Minaa* | Bonde karibu na Makkah na mahali patukufu wanapokwenda kulala wanaofanya Hajj |

| | |
|---|---|
| | kutekeleza baadhi ya vitendo vya fardhi za Hajj. |
| *Muakkadah* | Iliyosisitizwa. Mfano Sunnah iliyosisitizwa au Swalaah zilosisitizwa za kabla ya Swalaah na baada ya Swalaah za fardhi. |
| *Mustahabb* | Inapendekezeka kutendwa. |
| *Muzdalifah.* | Sehemu tukufu wanapokesha Waislamu katika ʻibaadah ya Hajj ipo baina ya *ʻArafah* na *Minaa*. |
| *Naafilah* | Vitendo vya ʻibaadah ambavyo havikufaridhishwa na Allaah (سبحانه وتعالى) bali ni ambavyo Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم)amevitenda katika Sunnah zake, mfano Swalaah ya *Dhwuhaa, Witr, Tahajjud*, kufunga Jumatatu na Alkhamiys, *Ayyaam Al-Biydhw*, kutekeleza Hajj mara ya pili na ʻUmrah n.k. |
| *Namirah* | Msikiti uliopo *ʻArafah*. |
| *Nifaas* | Damu ya uzazi. |
| Nikaah | Kufunga ndoa. |
| *Niqaab* | Kifuniko cha uso wanachovaa wanawake Waislamu. |
| *Niyyah* | Kutia *niyyah* ya ʻamali fulani ambayo mahali pake ni moyoni na si kutamkwa. |
| *Qadhwaa* Na *Qadar* | Majaaliwa na Makadario yaliyoandikwa katika Lawhim-Mahfudwh |
| *Qubaa* | Msikiti wa mwanzo waliojenga Waislamu walipoingia Madiynah kutoka Makkah pamoja na Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم). |
| *Rukn Al-Yamaaniy* | Pembe katika *Al-Ka'bah* baina ya kona hiyo na ya *Al-Hajar Al-As-wad.* |
| *Sakaraat Al-Mawt* | Mateso ya mtu wakati anapofariki. |
| *Salafus-Swaalih* | Wema waliotangulia katika karne tatu za mwanzo alizozisifu Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). Karne ya kwanza ikiwa ni karne ya Maswahaba na mbili zinazofuatia ndio jumla ni tatu. |
| *Shariy'ah* | Shariy'ah au hukmu za Dini. |

| | |
|---|---|
| *Shawwaal* | Mwezi wa kumi katika kalenda ya Kiislamu |
| *Sunnah* | Mwenendo wa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) katika kauli na matendo, au jambo waliotenda Maswahaba akalinyamazia kwa kuwa amelikubali. |
| *Sunnat Al-Wudhuu* | Sunnah ya wudhuu, inayoswaliwa rakaa mbili baada ya kuchukua wudhuu. |
| *Suwratul-Ikhlaasw* | Suwrah Namba 112 katika Qur-aan. |
| *Suwratul-Kaafiruwn* | Suwrah Namba 109 katika Qur-aan. |
| *Swahaabah* | Wanaume walioishi na kumuona Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). |
| *Swahaabiyaat* | Wanawake walioishi na kumuona Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم). |
| *Swahiyh* | Sahihi. |
| *Tahajjud* | Swalaah inayoswaliwa usiku baada ya mtu kuamka usingizini kama ni 'amali ya naafilah. |
| *Tahiyyat Al-Masjid* | Swalaah ya rakaa mbili anayoswali mtu anapoingia tu Msikitini kwa ajili ya kuamkia Msikiti. |
| *Tahliyl* | Kumpwekesha Allaah: *Laa ilaaha illa-Allaah*. |
| *Tahmiyd* | Aina zote za kumhimidi Allaah mfano kusema AlhamduliLLaah. |
| *Takbiyr* | Kumtukuza Allaah: *Allaahu Akbar*. |
| *Takbiyr* | Kusema *Allaahu Akbar* (Allaah Mkubwa). |
| *Takbiyrah* | *Takbiyr*. Kusema *Allaahu Akbar* (Allaah Mkubwa). |
| *Talbiyah* | Du'aa ya Muislamu anayosema anapoingia katika Ihraam baada ya kutia niyyah. |
| *Tamattu'* | Aina ya Hajj ya kustarehe (mapumziko) kwa kuwa anatekeleza 'Umrah kwanza kisha anajitoa katika Ihraam kisha anatekeleza Hajj. Mwenye kuhiji hutakiwa kuchinja na awe hakufika Makkah na mnyama huyo. |
| *Tarwiyah* | Tarehe 8 ya Dhul-Hijjah. |

| | |
|---|---|
| *Tasbiyh* | Aina zote za kumtakasa Allaah mfano Subhaana-Allaah, *Subhaana Allaahi wa Bihamdihi, Subhaana-Allaahi Al-'Adhwiym* n.k. |
| *Tawfiyq* | Kuwezeshwa na Allaah (سبحانه وتعالى) kutekeleza jambo. |
| *Twaaf Al-Ifaadhwah* | *Twawaaf* ya Hajj ambayo ni moja nguzo katika taratibu za Hajj. |
| *Twawaaf* | Mzunguko katika *Al-Ka'bah*. |
| *Twawaaf Al-Quduwm* | *Twawaaf* ya kuingia (mwanzo unapowasili) Makkah ambayo inatekelezwa na mwenye kuhiji Hajj ya *Al-Qiraan* na *Al-Ifraad* kama ni kitendo cha Sunnah. |
| *Twawaaf Al-Wadaa'i* | *Twawaaf* ya kuaga |
| *Twawaaf At-Tatwawwu'* | *Twawaaf* ya kupenda mtu kufanya kama ni 'amali njema. Hutekelezwa pale mtu kila anapoingia Masjid Al-Haraam kabla ya kuketi Msikitini. |
| *Uhud* | Jabali lilioko Madiynah umeitwa hivyo kutokana na vita vilivyotokea hapo. |
| *'Umrah* | Hajj ndogo inayofanywa kwa *Twawaaf* na kuswali *Maqaam Ibraahiym* na *As-Sa'-y* pekee. Au mtu kuitekeleza kwa ajili yake pekee bila ya kuwa katika misimu ya Hajj. |
| *Waswiyyah* | Wasiya anaopaswa Muislamu kuandika kabla ya kufariki dunia. |
| *Yawm An-Nahr* | Siku ya kuchinja yaani tarehe 10 ya Dhul-Hijjah ambayo ni sikukuu ya *'Iyd Al-Adhw-haa*. |